BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

Simu Nam. + 255 24 2230602/1
Fax Nam. + 255 24 2230215
Tovuti: www.zanzibarassembly.go.tz

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR
Barua Pepe: zahore@zanlink.com

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA KUSIMAMIA OFISI ZA VIONGOZI WAKUU WA KITAIFA KUHUSIANA NA BAJETI YA OFISI YA MAKAMO WA PILI WA RAIS KWA MWAKA 2018/2019

---

Mheshimiwa Spika:

Awali ya yote naanza kutoa shukurani zangu za dhati kwa Mwenyezi Mungu Mtukufu, Muumba wa viumbe vyote ambaye ndiye mwenye kukirimu uhai kwa viumbe ambavyo vipo chini ya milki yake. Pia, naendelea kuchukuwa fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa neema ya uhai na afya njema ambayo ametujaalia na kutuwezesha leo hii kuweza kusimama mbele ya Baraza lako tukufu kuwasilisha hotuba ya Kamati yetu na nyinyi wajumbe wenzetu wa Baraza hili kuendelea kutusikiliza kwa makini. Hii ni dalili tosha kwamba wajumbe wa Baraza lako tukufu wana nia ya dhati ya kuwatumikia wananchi kwa lengo la kuishauri Serikali na hatimaye Serikali nayo iweze kutekeleza majukumu iliyojipangia kwa dhamira ya kupeleka mbele maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar.

Pia, sina budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumpa afya njema, nguvu, hekima na busara Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. ***Dkt. Ali Mohammed Shein,*** na kumuwezesha kuwatumikia wananchi katika utumishi uliotukuka zaidi. Hivyo sisi sote tuliopo chini yake hatuna budi kuiga na kufuata nyayo zake za utumishi uliotukuka kwa wananchi wetu. Tunamuomba Mwenyezi Mungu amuongezee hekima na busara zaidi Mheshimiwa Spika na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishina Viongozi wote atuongoze katika kuwatumikia wananchi wetu ambao wana imani kubwa na Serikali yao kwani huo ni wajibu wetu sote kuwatumikia kwa utumishi uliotukuka na wenye uadilifu zaidi.

**Mheshimiwa Spika:**

Kwa namna ya pekee natumia nafasi hii kumshukuru na kumpongeza sana Makamu wa Pili wa Rais, **Mhe. Balozi Seif Ali Iddi** kwa kuwa mstari wa mbele kuwatumikia wananchi katika mambo mbali mbali. Ukweli ni kwamba kila linapotokea jambo lolote linalohusu mustakabali wa nchi yetu anachukuwa hatua za haraka kulitatua. Utaratibu huo wa kazi ambao anautekeleza ndio sababu iliyowafanya wananchi wawe na imani kubwa na Balozi Seif na kuamini kuwa ni kiongozi mchapa kazi muwadilifu.

Aidha, nitoe shukurani za dhati kwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, **Mhe. Mohammed Aboud Mohammed** kwa utendaji wake bora katika kazi zake za kila siku, sambamba na Mhe. Naibu Waziri wa Wizara ya Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, **Mhe. Mihayo Juma N'hunga**, kwa namna ya pekee wanavyoshirikiana na Kamati hii ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kwa muda wote wa kazi za Kamati. Hadi leo hii kufikia kuisoma Hotuba ya Kamati ya Kusimamia Ofisi ya Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusiana na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, tumefanya nao kazi bega kwa bega kwa muda wote wa shughuli za Kamati kwa mwaka mzima bila ya kuchoka, na pale inapotokea dharura ya kukosekana kwa ajili ya majukumu mengine ya Kitaifa, huwa wanaiarifu Kamati yangu na kupanga utaratibu mwengine uliobora ambao utaiwezesha Kamati hii kufanya kazi zake bila kukosa.

**Mheshimiwa Spika:**

Nitakuwa mchoyo wa shukurani iwapo nitamaliza kusoma maoni haya ya Kamati ya Ofisi ya makamu wa Pili wa Raisi ya Bajeti kwa mwaka wa fedha **2018/2019**, bila ya kuwapongeza na kuwashukuru watendaji wote wa Ofisi hii, wakiongozwa na Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, kwa kuonesha ushirikiano mkubwa kwa Kamati yangu katika kipindi chote cha mwaka wa **fedha 2017/2018**, wakati Kamati yangu ikiendelea na jukumu la kuisimamia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa lengo la kuhakikisha utekelezaji bora wa Bajeti kwa kuzingatia nidhamu ya matumizi ya fedha kwa mujibu wa Sheria tulizojiwekea sisi wenyewe.

Aidha, kwa masisikitiko makubwa, nichukue fursa hii pia kuwapa pole Wajumbe wa Baraza na wananchi wetu wote ambao kwa namna moja au nyengine kwa mwaka **2017/2018**, walipata misiba mbali mbali, ikiwa pamoja na maafa yanayotokana na mvua zinazoendelea kunyesha, vifo,ugonjwa na maafa mbalimbali ya kibinaadamu, niwaombe wawe na moyo wa subira kwani hiyo ni kazi ya Mwenyezi Mungu.

Pamoja na hayo tunapaswa kuchukuwa tahadhari na kujikinga na maafa mbali mbali ambayo yanaweza kutokea kwani kufanya hivyo sio tu kusaidia Serikali kutekeleza majukumu mengine iliyojipangia bali pia kusaidia familia zenyewe kuepukana na maafa au majanga hasa yanayotokana na mabadiliko ya hali ya tabianchi yakiwemo mafuriko ambayo yamekuwa ni tatizo katika maeneo mengi ya Zanzibar na jambo ambalo huziweka familia nyingi wakati mgumu.

**Mheshimiwa Spika:**

Nianze kuaianisha kwa muhtasari majukumu ya msingi ya Wizara hii ambayo ni Uratibu wa Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Shughuli zote za Muungano kwa upande wa Zanzibar ikiwa ni pamoja na Uratibu wa baadhi ya Miradi ya maendeleo inayosimamiwa kwa pamoja kati ya SMZ na SMT ndani ya Zanzibar.

Aidha, majukumu mengine ya msingi ni pamoja na Kusimamia na Kuratibu Shughuli za SMZ Dar es salaam, Kusimamia Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa na Kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa, Kuratibu Masuala ya Kukabiliana na Maafa, Kusimamia na Kuratibu Shughuli za Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Shuhuli za Watu wenye Ulemavu, Kusimamia Masuala ya UKIMWI, Kuratibu na Kudhibiti Dawa za Kulevya, Kusimamia Shughuli za Tume ya Uchaguzi na Baraza la Wawaklishi.

**Mheshimiwa Spika:**

Kwa mujibu wa utaratibu wa kibajeti kwa mwaka wa fedha **2018/2019**, Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, inaliomba Baraza lako tukufu kuidhinisha jumla ya **Tsh. 57,142,200,00**0, ambazo zimetegwa kwa ajili ya shuhuli zake za kawaida na Miradi ya maendeleo. Kimsingi shughuli zote kwa mwaka wa fedha **2018/2019** ambazo zitakuwa **Mafungu** kuu tano, ambazo ni **Fungu C01**- Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais**, Fungu CO2-** Baraza la Wawaklishi, **Fungu C03**- Tume ya Uchaguzi, **Fungu C04**- Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti Dawa ya Kulevya, na **Fungu C05**-Tume ya Ukimwi.

**Mheshimiwa Spika:**

Baada ya kueleza Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili kwa ujumla, sasa kwa idhini yako naomba nitoe maoni ya Kamati yangu, yajikite kwa kila taasisi kwa mujibu wa Programu, shughuli na huduma zilizopangwa kutekelezwa ambapo kwa mwaka huu wa fedha Ofisi ya Makamu wa Pili kwa ujumla wake imepanga kutekeleza Programu kuu kumi na moja (11) na Programu ndogo ishirini na tano (25) kama ifuatavyo:

## OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS

**Mheshimiwa Spika:**

Kamati yangu imepitia fungu baada ya fungu, kwa ajili ya kupata ufafanuzi na hatimae kuridhia jumla ya fedha zote ambazo zinakusudia kutekeleza jumla ya Programu kuu tatu (3), nazo ni:

1. Uratibu wa Shughuli za Makamu wa Pili wa Rais,
2. Uratibu wa Shughuli za Serikali,na
3. Uendeshaji na Uratibu wa Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais.

Aidha, lengo la Programu Kuu zote tatu ni pamoja na kuimarisha utendaji wa kazi wa Ofisi ya faragha ya Makamu wa Pili, ambao ni Uhimili wa jamii katika Kukabiliana na maafa kabla na baada ya kutokea, Kuwa na Sherehe za Kitaifa zenye hadhi pamoja na kudumisha historia na kumbukumbu za Viongozi Wakuu wa Kitaifa,Kuratibu na usimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi kwa Taasisi zote za Serikali, Kuimarisha utoaji wa huduma kwa Taasisi za SMZ kwa upande wa Tanzania Bara, Kuhakikisha upatikanaji wa haki kwa Watu Wenye Ulemavu, Kusimamia utekelezaji wa mpango wa maendeleo wa kunusuru kaya maskini (TASAF III), Usimamizi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi, Kuimarisha Mazingira bora ya kufanya kazi na usimamizi wa shughuli za Ofisi wa Makamu wa Pili wa Rais kwa Unguja na Pemba.

**Programu ya Uratibu washughuli za Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais**

**Mheshimwa Spika:**

Ofisi ya Makamu wa Pili ndio dira ya Serikali yetu kwani ni kiungo kikubwa sana baina ya Serikali na wananchi wake, kupitia Idara hii ya Huduma za Makamu wa Pili wa Rais ambayo, moja ya jukumu lake la msingi ni kupokea na kushuhulikia malalamiko na kutafuta utatuzi wa migogoro mbali mbali inayowasilishwa kutoka kwa wananchi kama tulivyoelezea hapo mwanzo kwamba Makamo wa Pili wa Rais Mheshimiwa Balozi Seif amekuwa akichukua hatua za haraka sana kutatua migogoro mara tu inapowasilishwa kwake. Idara hii ni miongoni mwa Idara muhimu kwenye wizara kwa hivyo, Kamati yangu inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kushughulikia na kuyapatia ufumbuzi malalamiko 22 kati ya 35 yaliyowasilishwa na wananchi.
Kamati imefurahishwa na utatuzi wa migogoro na matumaini yetu migogoro iliyobaki itatuliwa kabla kumalizika mwaka 2018.

Kamati inasisitiza na kushauri wizara kabla ya malalamiko kuyapeleka kwa Mheshimiwa Makamo wa Pili wa Rais wayape uzito pamoja kuongeza kasi ya utatuzi wa malalamiko hayo kwani kuwepo kwa malalamiko mengi hakutoi taswira njema kwa Serikali.
Hivyo kamati imefurahishwa na ongezeko zima la Bajeti katika kifungu hiki wa ajili ya kuweza kutekeleza majukumu yao vyema na kwa ufanisi zaidi.

**Programu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali**

**Mheshimiwa Spika:**

Ili kukamilisha utekelezaji wa Programu kuu hii yenye Programu ndogo saba kama ambavyo inaonekana kwenye hotuba ya wizara na kwa mujibu wa fedha ambazo wizara inaomba kuidhinishwa, zinatarajiwa kutumika kutekeleza Programu ndogo zifuatazo:

a) Kukabiliana na Maafa,
b) Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na kuwaenzi Viongozi Wakuu wa Kitaifa,
c) Shughuli za SMZ,
d) Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar-Dar-es-Salaam,
e) Usimamizi wa Masuala ya Watu wenye Ulemavu,
f) Usimamizi wa Mazingira,
g) Uratibu wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

**Mheshimiwa Spika:**

Kila Programu kati ya hizo ina umuhimu wake kwa nafasi yake. Hata hivyo naomba nizungumzie Programu ya kukabiliana na maafa tunaona kwamba Kamisheni ya kukabiliana na maafa ina majukumu ya kuratibu masuala ya kukabiliana na maafa pamoja na kusimamia utekelezaji wa mipango ya kukabiliana na maafa wakati wa maafa ya asili au dharura yanapotokezea na kutoa amri na maelekezo yanayofaa. Katika utekelezaji wa mpango huo Kamisheni imekuwa ikichukua juhudi mbali mbali kwa kuanzisha kamati za kukabiliana na maafa katika ngazi za wilaya na shehia, kuanzisha maghala na vifaa vya kukabiliana na maafa, vituo vya uokozi katika maeneo mbalimbali, vituo vya operesheni na masuala ya dharura pamoja na kutoa elimu kupitia vyombo vya habari ambapo lengo la kamisheni ni kulinda maisha ya watu na mali zao.

Kamati yangu inatoa pongezi nyingi kwa Kamisheni ya Kukabiliana na Maafa kwa juhudi wanazoendelea kuzichukua kuhakikisha wanawafikia kwa kuwapa huduma za msingi wananchi wote pale wanaopatwa na maafa kwa Unguja na Pemba. Hata hivyo pamoja

na juhudi kubwa zinazochukuliwa na Serikali katika kukabiliana na maafa tunaishauri Serikali kuyapatia ufumbuzi maeneo sugu yanayojaa maji na kusababisha mafuriko kila siku.
Vilevile, Kamati inatarajia kupata maelezo kuhusu mikakati ya Serikali ya kuhakikisha maeneo hayo yanapatiwa ufumbuzi na wananchi hawasumbuki kutokana na mvua zinazoendelea na kusababisha kujaa maji katika maeneo hayo.

Kamati imeona kwamba bado Kamisheni inakabiliana na changamoto mbali mbali zikiwemo kutosimamiwa ipasavyo kwa sheria na kanuni mbali mbali zinazohusiana na masuala ya kukabiliana na maafa, zikiwemo sheria za mipango miji. Pia kutosimamiwa ipasavyo udhibiti wa vyanzo vya maji na utaratibu wa ujenzi na kupelekea watu kujenga mabondeni au chini ya milima.

Aidha, elimu ya kukabiliana na maafa kwa jamii inaonekana bado ni ndogo, kutokuwepo kwa mfumo maalumu wa kukabiliana na maafa utakaosaidia katika kujikinga, kujiandaa kukabiliana na maafa. Pia kamati imebaini kuwa wananchi wana tabia ya kujenga kwenye maeneo hatarishi, sambamba na tabia ya kutupa taka katika mitaro na kusababisha kuiziba mitaro inayopitisha maji wakati wa mvua.

Hivyo, matumaini Kamati inatarajia kuona kuwa bajeti iliyoombwa kwa mwaka kwa fedha 2018/2019 itaweza kutatua baadhi ya changamoto hizo ambazo Kamisheni inakabiliana nazo.

**Mheshimiwa Spika**:

Suala jengine katika Programu hii ambalo Kamati yangu imeliangalia kwa umakini sana na kulipa uzito wa aina yake ni suala la Uratibu wa Shughuli za SMZ, na hasa ikizingatiwa katika masuala ya kero na changamoto za Muungano. Ukweli ni kwamba licha ya kuwepo kwa Kamati ya pamoja ya Mawaziri wa SMZ na SMT kwa ajili ya utatuzi wa kero za Muungano na kwamba zipo baadhi ya kero ambazo zimeshapatiwa ufumbuzi wake lakini bado kuna baadhi ya kero nyengine ambazo hazijatatuliwa licha ya kuwa ni za muda mrefu lakini Kamati ya pamoja ya pande zote mbili inaendelea kuzishughulikia ili wananchi wa pande zote mbili za muungano waweze kufaidika na matunda ya Muungano huu ambao waasisi wake waliuanzisha na kuturithisha sisi vizazi vyao kwa nia njema kabisa.

Hivi karibu tulisikia mjada unaohusiana na uingizwaji wa sukari inayozalishwa na kiwanda cha Mahonda cha Zanzibar kwenye soko la Tanzania bara na manung'uniko ya wafanya biashara wa Zanzibar wanaopeleka biashara zao Tanzania Bara kulipishwa

ushuru mara mbili na kwamba wapo baadhi ya wana siasa walilichukulia kwa uzito mkubwa Masuala ya wafanyabiashara wa Zanzibar kulipa ushuru mara mbili wanapoingiza biashara zao Tanzania bara.
Pamoja nakwamba Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeratibu vikao 19 vya mashirikiano baina SMT na SMZ, bado inahitaji kuongeza kasi ili kuweza kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo zinazohusu Muungano wetu. Kamati kupitia Bajeti ya 2018/2019 inaishauri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kuhakikisha kuwa vikao vya uratibu wa Masuala ya Muungano vinafanyika kwa lengo la kuendelea kutatua changamoto zilizopo ili kuepusha changamoto hizo kuengezeka zaidi.

**Mheshimiwa Spika:**

Kamati inatoa wito kwa Watanzania wote kwa pamoja tuiamini Kamati ya pamoja ya mawaziri wa pande zote mbili yaani ya SMT na SMZ, ambayo inafanya kazi nzuri iliyokabidhiwa na Viongozi wetu Wakuu ambao wanazishughulikia changamoto hizo lakini pamoja na hayo ni vyema ukaandaliwa utaratibu wa mfumo maalumu wa utoaji wa taarifa kuhusu mafanikio yaliofikiwa katika kila kikao kinachojadili masuala hayo
Kamati inaamini kwamba kuwepo kwa mfumo wa kuwapasha habari wananchi wetu utatoa mwanga na muelekeo kwa jamii juu ya Serikali yetu zinavyofanya bidii ya kuzipatia ufumbuzi changamoto zinazojitokeza na pia zitasaidia uelewa kwa wananchi kuwafamu baadhi ya wanasiasa ambao hawautakii mema Muungano wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Programu nyingine muhimu ambayo Kamati imeifanyia kazi ni suala la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa miradi ya TASAF III.

Kamati imeona kwamba katika Mpango wa kunusuru Kaya Maskini (TASAF III), Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ imeweza kuratibu shughuli mbali mbali kwaUnguja na Pemba kwa mafanikio makubwa. Fedha zilizopangwa kufika katika Kaya hizo zilifika kwa wakati. Kamati inaipongeza Idara kwa kutelekeza mradi huu kwa ufanisi wa hali ya juu na kuweza kupunguza utegemezi kwa wanakaya masikini ambao wameweza kuibua miradi yao mbali mbali kama vile ujenzi wa mabwawa ya kufugia samaki na upandaji wa miti ya kudumu na kilimo cha mboga mboga.

Kwa ujumla katika mwaka wa fedha 2017/2018 mradi wa TASAF III, umeweza kungatua baadhi ya wanakaya maskini kutoka katika umaskini uliokithiri na kuweza kujitegemea

wenyewe hivyo Kamati imepata imani kubwa juu ya kuwepo na kuendelea kwa mradi huo.

Kamati inaamini uwepo wa miradi hiyo ni msaada mkubwa kwa wanakaya hao kuweza kujinasua na umasikini uliokithiri kwani imewawezesha kujiajiri wenyewe.

Kamati inaamini kwamba katika bajeti ya mwaka 2018/2019, fedha zilizopangwa katika kutekeleza miradi hiyo itazidi kuzishughulikia kwa kina kaya hizo ili ziweze kujitegemea.

**Mheshimiwa Spika:**

Programu nyengine ndogo iliyo kwenye Progamu Kuu ya Uratibu wa Shughuli za Serikali, ambayo kamati imeona nayo ni muhimu kupewa mazingatio ya kipekee, ni juu ya Progamu ya Shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar-Dar-es Salaam. Kwa lugha nyepesi tunaweza kusema kuwa Idara ya Uratibu wa Shughuli za SMZ-Dar-es-Salaam, ndiyo kioo cha Serikali yetu kwa upande wa Tanzania bara. Idara hii inajukumu kubwa la kuziunganisha taasisi na wizara za Serikali zetu za SMZ na SMT ambapo kila shughuli za kiserikali zinazofanyika Tanzania bara, zinapaswa kuratibiwa na Ofisi hii.
Napenda kuchukua fursa hii kuipongeza kamati ya pamoja ya mawaziri wa pande zote mbili nazo ni SMZ na SMT kwa bidii na uwadilifu mkubwa wanaofanya katika kutekeleza wajibu wao wa kuzitafutia ufumbuzi baadhi ya changamoto na kero za muungano zilizopo

**Mheshimiwa Spika**:

Ilikuwa ni changamoto ya muda mrefu kwa Idara hii, kuhusu hali mbaya ya jengo ambalo ni Ofisi ya Uratibu wa SMZ iliyopo Dar-es-salaam, Kamati inaipongeza ofisi ya Makamu wa pili kwa kutumia bajeti ya 2017/2018 kwa kufanya kazi nzuri ya matengenezo ya sehemu ya jengo hilo ili liendane na hadhi ya Idara yenyewe.
Aidha, Kamati yangu imefarajika na inaishukuru Serikali kupitia Bajeti hii kuweza kutenga fedha za kutosha kwa ajili ya kulifanyia matengenezo makubwa hadi kuliezeka jengo hilo ili liendane na hadhi ya Ofisi hiyo, Ukitilia maanani eneo na mazingira yanazozunguka Ofisi hiyo, hasa ukizingatia, jengo hilo hutumika na kiongozi wetu Mkuu, Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, anapokuwa na vikao na mabalozi au viongozi wengine wakuu wa Kitaifa na Kimataifa

**Mheshimiwa Spika:**

Kutokana na unyeti wa Idara hii, na maingiliano yake yanayotokea baina ya watendaji wa Idara hiyo na idara nyengine za SMZ, SMT pamoja na Viongozi wengine wa kidiplomasia, Kamati inaipongeza Idara kwa kuwapatia mafunzo watendaji wake kwa lengo la kuwajenga uwezo katika fani mbali mbali. Kamati inasisitiza suala la mafunzo liwe ni la kuendelea kwa watendaji wengine kwa lengo la kuimarisha Ofisi,

**Mheshimiwa Spika**:

Programu nyengine ambayo Kamati yangu inaipa uzito katika Bajeti hii ni Programu ya Kuimarisha Ujumuishaji wa Watu Wenye Ulemavu. Moja ya jambo muhimu kwa watu wenye ulemavu ni ushirikishwaji katika harakati mbali mbali za maendeleleo kwa mujibu wa hali na uwezo wao. Kwa kuwa ni jukumu la Idara ya watu wenye ulemavu kufuatilia na kusimamia haki na fursa za watu wenye ulemavu katika jamii, Suala kubwa la kuzingatiwa ni mahitaji maalum kwa watu wenye ulemavu katika haki zao za msingi za kibinaadamu kama vile elimu ,afya na ajira ni jambo la msingi.

Kamati yangu inasikitishwa sana na hali ya watu wenye ulemavu kwa namna wanavyokosa mahitaji ya msingi kutokana na kutopewa kipaumbele kwa mambo yao mbali mbali yanayowagusa kama walemavu kwenye sekta za huduma, na hata uapatikanaji wa haki kwenye vyombo vya sheria.

Tukianza na miundo mbinu ya majengo mengi ya umma imekuwa ni changamoto kwa walemavu kuweza kuyafikia na kupata huduma kutokana na kukosekana kwa njia maalum za kupita kwa mujibu wa hali zao.

Mfano, hata jengo hili tukufu la watunga sheria limejengwa bila kuwazingatia wenzetu wenye mahitaji maalum.Kwa kweli huu ni msiba mkubwa.
Aidha, Sekta ya elimu nayo imekuwa ni mtihani mkubwa kwa watu wenye ulemavu, licha ya Sera ya elimu ya mwaka 2006 kutambua elimu kuwa ni haki yao ya msingi,lakini hali halisi haiko hivyo, kwani kumekuwa na uhaba mkubwa wa Walimu wenye sifa za kufundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum na pia kuna upungufu mkubwa wa vifaa vya kufundishia, matokeo yake imekuwa mzigo mkubwa kwa walimu wachache wenye kufundisha bila nyenzo.

Vile vile Sera ya elimu imekuwa ikikinzana na Sheria ya Elimu ya Mwaka 1982 ambayo haikuweka mkazo kwa watu wenye ulemavu.

Kamati inaipongeza sana Idara kwa kuweza kuandaa mkakati wa kupitia Sheria kwa lengo la kuandaa miongozo itakayosaidia watu wenye ulemavu kupata haki zao za msingi.

Kamati yangu inaishauri Idara ya Watu Wenye Ulemavu kwa kushirikiana na wizara ya elimu kuiga mfano mzuri wa skuli binafsi ya JABAL HIRAA ya Fuoni kuhusu namna ya kuwashirikisha walimu wote katika mafunzo ya elimu mjumuisho na hata wanafunzi wasiokuwa walemavu wafundishwe elimu hiyo tokea wadogo. Kwani kuwafundisha watoto wote hata wasiokuwa walemavu itakuwa ni faraja kubwa hata kwa familia pale inapotokea kuzaliwa mtoto ambaye ana tatizo la kuzungumza. Hali hiyo inaweza kusaidia ufumbuzi wa changamoto nyingine kwa watu wenye mahitaji maalum.

**Mheshimiwa Spika:**

Sekta ya afya nayo imekuwa ni kizungumkuti kwa watu wenye mahitaji maalum wanapokwenda kutaka huduma wanasumbuka sana kuzifikia huduma za kitabibu kutokana na miundo mbinu ya hospitali zetu na vituo vya afya. Lakini hata wale wanaoweza kuzifikia mara nyingine hukumbana na mkanganyiko baina yao na matabibu kutokana matabibu hao kutoelewa lugha ya alama na pia kutokuwepo kwa wakalimani katika maeneo hayo. Jambo hilo ni kikwazo ambacho pia watu wenye ulemavu wanakabiliana nacho na hatimaye kukosa huduma wanayoitegemea.

Licha ya kwamba Idara ya watu wenye ulemavu inajitahidi kuwapatia huduma watu wenye ulemavu lakini wamekuwa wakikosa baadhi ya mahitaji hayo ya msingi.
Jambo jingine kwenye sekta ya afya ni kukosekana kwa viungo bandia uhaba wa dawa za kupaka kwa walemavu wa ngozi na kukosekana kwa madakatari bingwa na huduma bora kwa walemavu wa ngozi ambao wamepata SARATANI YA NGOZI n.k.
Kamati inaipongeza sana idara ya watu wenye ulemavu kwa kuanzisha utaratibu wa kuwapatia bima za afya watu wenye ulemavu ukweli ni jambo la kupongezwa kamati inasisitiza huduma hii iweze kupatikana kwa walemavu wote.

Kamati yangu inaishauri Serikali iongeze nguvu zake za kibajeti kwa Idara ya watu wenye ulemavu kwa kushirikiana na Wizara ya Afya,Wizara ya Elimu, pamoja na Wizara Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ ambopo skuli na vituo vya afya vimegatuliwa kuisaidia Idara ili iweze kukidhi majukumu na mahitaji mbali mbali ya watu wenye ulemavu.

Suala jingine ambolo ni sugu kwa watu wenye ulemavu ni suala la udhalilishaji dhidi yao. Ni ukweli kwamba suala la udhalilishaji kwa watu wenye mahitaji maalum lilikuwa linaongezeka kila siku. Kamati inaishukuru Serikali kupitia Wizara ya kazi, Uwezashaji Maendeleo ya Wanawake, Wazee na Watoto kwa kuyafuatilia kwa karibu sana malalamiko dhidi ya watu wenye ulemavu na kuhakikisha sheria inachukuwa mkondo wake na hatua kali zinachukuliwa dhidi ya wale wote wanaohusika na tatizo hili la udhalilishaji wa watu wenye ulemavu.

**Mheshimiwa Spika:**

Kamati yangu inaipongeza sana Serikali kwa kuona umuhimu wa kuwa na Baraza la watu wenye ulemavu ambalo linaweza kutumika kama jukwaa lao la kupitishia mahitaji yao ya msingi. Baraza limeweza kutumika kama sehemu muhimu ya kujadili na kutatua changamoto mbali mbali zinazohusu mahitaji ya watu wenye ulemavu.
Kamati inapongeza Wizara kwa kuwaongeza Bajeti ya Idara ya Watu wenye Ulemavu kupitia Programu ndogo ya usimamizi wa watu wenye ulemavu, ingawa bado Kamati inaamini Bajeti hiyo ni ndogo kwa mujibu wa mahitaji ya Idara hiyo, na uhalisia wa shughuli zake za kila siku. Hivyo bado tunaiomba Serikali kuweza kuangalia Bajeti ya Idara hiyo kwa jicho la huruma zaidi.

## KAMISHENI YA MAZINGIRA

**Mheshimiwa Spika,**

Kutoka na mabadiliko ya kiwizara kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais imeongeza Programu ndogo Mbili ya Usimamizi wa Mazingira na Uratibu wa Mazingira na Tabianchi. Kupitia programu hizo ambazo zina lengo la kuimarisha hali ya mazingira Zanzibar na kuiandaa jamii kujihami kutokana na mabadiliko ya tabianchi. Kamati inaamini kwamba Idara ya Mazingira na Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira (ZEMA) zina majukumu makubwa ya kuhakikisha kwamba uhifadhi wa mazingira unapewa uzito unaostahiki na kila mmoja wetu. Suala la taaluma kwa wananchi juu ya umuhimu wa uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni muhimu.

Kwa kuwa Taasisi hii pia inahusika na tathmini ya hali ya mazingira kabla ya kuanza kwa miradi mbali mbali inapaswa kujipanga vizuri kuhakikisha kwamba kila mradi unaotakiwa kufanyiwa tathmini hiyo unafanyiwa kwa kufuata taratibu na kwa wakati ili kuepuka athari kwa wananchi na kuhakikisha miradi hiyo inatoa tija badala ya kuleta athari za kimazingira kwa wananchi.

Aidha, Kamati inazishauri taasisi zinazosimamia mazingira zisimamie majukumu yake zihakikishe kuwa utaratibu wa malipo unawekwa vizuri ili mapato ya Serikali yasiweze kupotea ikiwa ni pamoja na kuandaa kanuni za malipo ili kuwa na utaratibu mmoja kwa watu wote. Aidha, suala la kuwa na mfumo wa kieletroniki kwa kwa ajili ya kuweka kumbu kumbu za kimazingira ni muhimu.

Vilevile, Kamati inashauri kuanzishwa vikundi vya kuhifadhi mazingira kuvindeleza na kuvipatia msaada hasa kwa yale maeneo ambayo bahari imekuwa sehemu kubwa ya ardhi kama Msuka kwa Pemba na ukanda wote wa utalii wa Mashariki ya Kisiwa cha Unguja. Aidha; Sera ya mazingira ambayo ni muongozo wa masuala hayo inashauriwa itafsiriwe kwa Kiswahili kwani wengi wa walengwa wa sera hiyo ni wazungumzaji wa lunga ya Kiswahili.

Pia, Kamati inashauri jitihada za makusudi ziandaliwe na kuwekewa mikakati kuhakikisha kwamba wakandarasi wa ujenzi wa barabara wanapanda miti mara baada ya kukamisha kazi ya uchimbaji wa kifusi kwa ajili ya ujenzi ili kuepusha uharibufu wa mazingira.
Kamati inaamini kwamba bajeti ya mwaka 2018/2019 itatumika vizuri na kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa.

## TUME YA MADAWA YA KULEVYA

**Mheshimiwa Spika:**

Suala la madawa ya kulevya ni suala la kitaifa, na vita vyake inahitaji uzalendao wa hali ya juu. Bajeti hii kupitia Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya, imetenga fedha kwa lengo laa kutekeleza utekelezaji wa shughuli zote za Tume, kupitia Programu kuu mbili ambazo ni pamoja na **Programu ya Udhibiti wa dawa za kulevya** na **Programu ya Uendeshaji na Uratibu wa Tume ya Dawa za Kulevya**.

**Mheshimiwa Spika:**

Bajeti ya Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa dawa za Kulevya imeongezeka kwa mwaka **2018/2019**. Kamati yangu imekua ikifanya kazi kwa ukaribu na ushirikiano mkubwa na tume hii, hivyo inafahamu changamoto zake ambazo pia zinaambatana na ufinyu wa bajeti ambao ulikuwa ukiikabili Idara hii hapo kabla. Hivyo basi, kwa ongezeko hili la bajeti kwa mara hii ni imani ya kamati yangu kuwa, Tume itaweza kutekeleza majukumu yake ya msingi, kwa ufanisi zaidi kulinganisha na mwaka wa fedha unaomalizika.

**Mheshimiwa Spika:**

Geografia ya Visiwa vya Zanzibar, kulinganisha na uwezo wa kifedha na nyenzo za kufanyia kazi za Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa dawa za kulevya, inafanya Programu ndogo ya kudhibiti na Usambazaji wa Dawa za kulevya izidi kuwa ngumu kutokana na kuwepo kwa bandari bubu nyingi sana, mfano Mkoa wa kaskazini Pemba tu wana bandari bubu 168 ambazo zinaweza kutumika kwa uhalifu wa aina mbali mbali na hata uingizwaji wa dawa za kulevya. Ni ukweli usiofichika kupitia bandari zisizo rasmi, dawa za kulevya zinaweza zikaingizwa na udhibiti wa bandari hizo bado ni mdogo mno. Katika utekelezaji wa bajeti hii, ambayo Programu ndogo ya kudhibiti Uingizaji na Usambazaji wa Dawa za Kulevya imeongezewa fedha kwa mwaka wa fedha **2018/2019** kwa asilimia kubwa ukilinganisha na bajeti ya 2017/2018.

Kamati yangu inaamini, chini ya usimamizi mzuri wa Mkurugenzi wa Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa dawa za Kulevya, Programu hii itatekelezwa kwa ufanisi mkubwa kutokana na ongezeko kubwa la fedha. Pamoja na kwamba Kamati imeridhika na maelezo kuwa fedha nyingi katika hizo zinatumika kwa kununulia samani na uendelezaji wa ujenzi wa nyumba ya marekebisho ya tabia iliyopo Kidimni kwa hatua ya ujenzi wa ghorofa ya kwanza.

**Mheshimiwa Spika:**

Kwa kuwa vita dhidi ya madawa ya kulevya ni vita ya kitaifa, na inamgusa kila mwananchi, Kamati yangu inashauri pia, suala la kuihamasisha jamii juu ya athari ya dawa za kulevya, suala ambalo nalo limetajwa kama moja wapo ya eneo ambalo litafanyiwa kazi na Tume. Kamati inataka Serikali kulipa kipaumbele cha upekee jambo hilo, kwa lengo la kuwafikia wananchi walio wengi kupitia shehia zao. Sambamba na jitihada binafsi zinazochukuliwa na baadhi ya Viongozi mbali mbali wakiwemo wakuu wa Mkuu wa Mikoa na Wilaya kama vile Mkuu wa Mkoa wa Mjini Magharib-Zanzibar. Kamati yangu inawataka Viongozi wote kuwa mstari wa mbele katika vita dhidi ya dawa za Kulevya.

Vile vile Kamati imefurahishwa sana na jitihada za Tume ya Kitaifa ya Kuratibu na Udhibiti wa Dawa za Kulevya kutoa elimu kwa taasisi tofauti kama vile Mikoa na Jumuia zisizo za kiserikali (NGO), Mahakama na kwa Wakuu wa Wilaya ambao matunda yake yameanza kuonekena katika kufikia jamii kwa kuwaelimisha vijana wetu juu ya adhari za matumizi ya dawa za kulevya.

Kamati yangu inaamini kwamba ushindi utapatikana dhidi ya mapambano hayo ya vita vya madawa za kulevya. Iwapo tutashirikiana pamoja na kuondoa ugonjwa wa rushwa, muhali na kuoneana aibu ambalo ni tatizo kubwa kwenye vita hivi kwani muhali ni rushwa mbaya sana na kama hatukukaza kamba ya mapambano hayo Taifa litaangamia kwa kupoteza nguvu kazi kubwa tunayoitegemea. Wito wa Kamati yangu ni kwamba mapambano dhidi ya madawa ya kulevya iwe endelevu hadi pale ambapo wale wote wanaojihusisha na biashara hii ya dawa za kulevya waache kabisa.

## BARAZA LA WAWAKILISHI

**Mheshimiwa Spika:**

Kamati yangu imepitia fungu la Baraza la Wawakilishi na kuhoji na kupata ufafanunzi na hatimae kuridhia fedha zote ambazo zinakusudia kutekeleza jumla ya Programu kuu mbili (2). Lengo la Programu hizo ni kuhakikisha haki na utawala wa sheria unatekelezwa Zanzibar na kuweka mazingira mazuri ya kazi, kuwajengea uwezo wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na wafanyakazi wa Ofisi ya Baraza la Wawakikishi.

Kamati yangu inaipongeza sana Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kwa namna ambavyo wanavyojitahidi kutoa huduma stahiki na kwa wakati kwa wajumbe wa Baraza la Wawakilishi na watendaji wa baraza hilo hivyo kuweza kufikia malengo ya kuwepo kwa Baraza hili la kuwatumikia wananchi kupitia wawakilishi wao.

Kwa kuwa moja ya shughuli iliyopangwa kutekelezwa na Programu hii ni Kuendelea kuweka mazingira mazuri ya majengo na kumbi za mikutano pamoja na kutoa huduma bora kwa wajumbe ili waweze kutekeleza vyema majukumu yao,Kamati yangu inaiomba Ofisi ya Baraza la Wawakilishi kuweza kutilia maanani na kulipa uzito unaostahiki suala la kuimarisha kumbi za mikutano pamoja na Ofisi za watendaji wa Baraza la Wawakilishi, ukweli ni kwamba kwa sasa kumbi zetu haziko katika hali njema.Aidha; uhaba wa vitendea kazi kwa watendaji nayo ni changamoto katika Ofisi ya Baraza.

## TUME YA UCHAGUZI

**Mheshimiwa Spika:**

Tume ya Uchanguzi ina Programu mbili kuu ambazo zinatarajiwa kutekelezwa na Ofisi ya Tume ya Uchaguzi kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Programu hizo ni Uendeshaji wa shughuli za uchaguzi na Usimamizi wa Kazi za Utawala na Uendeshaji wa Shughuli za Tume ya Uchaguzi.Kamati yangu imepitia shughuli zote zinazokusudiwa kutekelezwa na

Ofisi ya Tume ya Uchaguzi kupitia Programu hizo na imeridhia kuidhinishiwa jumla ya fedha walizoomba ili waweze kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi.
Aidha, Kamati imeishauri Tume ya Uchaguzi kuwa makini katika utekelezaji wa malengo yake hasa katika suala zima la uajiri, Tume inapaswa kuzingatia watu wenye sifa stahiki ili kuajiri maafisa waaminifu katika utekelezaji wa majukumu yao.

## TUME YA UKIMWI

**Mheshimiwa Spika**:

Katika bajeti ya 2018/2019 Tume ya UKIMWI ina Programu kuu mbili nazo ni Kuratibu Muitiko wa Taifa wa UKIMWI na Utawala na Uendeshaji.
Kamati imefurahishwa na ongezeko la Bajeti katika Tume ya UKIMWI kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2017/2018 kamati katika mizunguko yake ya kazi za Kamati ilipata fursa ya kutembelea jumuiya za kiraia zinajihusisha na mapambano dhidi ya UKIMWI kwa Pemba.Aidha Kamati ilikutana Jumuiya wa watu wanaoishi na Virusi vinavyosababisha UKIMWI (ZAPHA+)-Pemba.

Kamati imefajika na jitihada zinazochukuliwa na Jumuiya hiyo katika harakati mbali mbali za kumbambana na kuzuia uwambukizaji mpya wa virusi vinavyosababisha UKIMWI. Hata hivyo Kamati imebaini kuwepo kwa changamoto kadhaa zinazorudisha nyuma harakati za jumuiya hiyo.

Ni matumaini ya Kamati kwamba ongezeko la Bajeti kwa Tume ya UKIMWI litasaidia kutatua baadhi ya changamoto hizo na kuwawezesha kusongambele katika harakati za kupambana na maambukizi mapya ya VVU hasa kwa kuwa Tume ya UKIMWI imejipanga kuwapatia ruzuku Jumuia hizo kwa ajili ya kusaidia katika kutoa elimu juu ya athari za hali hiyo. Aidha, Kamati imesisitiza umuhimu wa kutoa elimu katika televisheni na redio pamoja na matangazo katika mitaa ni jambo la kuzingatiwa na kuchukuliwa hatuwa ili kuokowa jamii kutokana maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI.

### MAPATO

**Mheshimiwa Spika:**

Bajeti hii imeeleza na kuchambua kwa uwazi kabisa juu ya shughuli zilizopangwa kufanyika, lakini sitakuwa nimetenda haki bila ya kugusia suala la mapato. Wizara ya Nchi Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, ni moja wapo ya Wizara zenye kukusanya mapato kupitia Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa pamoja na Idara na

Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kwa kuwa Serikali yetu bado ina mahitaji makubwa ya kuongeza vyanzo vyake vya mapato na kuongeza ufanisi wa utekelezaji wa Bajeti.
Kamati yangu inashauri Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa na Idara ya Mamlaka ya Usimamizi wa Mazingira kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato kwa kutumia fursa zilizopo Zanzibar kupitia huduma zinazotolewa na taasisi hizo.

**Mheshimiwa Spika:**

Kwa bajeti ya mwaka wa fedha **2017/2018**, Idara ya Sherehe na Maadhimisho ya Kitaifa inatarajia kupata Bajeti kwa ajili ya ununuzi wa vifaa inavyohitaji kwa ajili ya utoaji wa huduma zake kwa asilimia **100** kama inavyotarajiwa katika Bajeti ya mwaka **2018/2019.** Hivyo, Kamati yangu inashauri Idara kuona umuhimu huu wa Bajeti inayoipata, kuwa ni fursa ambayo wanaweza kuitumia kwa kutoa huduma kwa taasisi za Serikali, na watu binafsi wenye uhitaji wa huduma zao, kufanya hivyo kutaiongezea Idara ufanisi na mapato zaidi ambayo yataimarisha utekelezaji wa Bajeti ya Serikali kwa ujumla ambapo kwa mwaka wa fedha **2018/2019** imepanga kukusanya jumla ya **Sh. 13,500,000.**

Kwa upande wa Usimamizi wa Mazingira jumla ya shilingi 45,974,000 zimepangwa kukusanywa. Kamati inaishauri Taasisi za Usimamizi wa Mazingira kuongeza umakini katika usimamizi wa ukusanyaji mapato ili kuhakikisha malengo waliojipangia yanafikiwa na ikiwezekana kuvuka malengo hayo.

Kamati inaipongeza Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kuona kwamba Makadirio ya Mapato kuongezeka kutoka Tsh 32,521,000 mwaka wa fedha **2017/2018** hadi Tsh 59,474,000 kwa mwaka wa fedha **2018/2019.**

Aidha. Kamati yangu inaishauri Wizara kuimarisha vyanzo vya kodi ya majengo ya maduka yaliyokuwepo Mwanakwerekwe ili kuweza kuongeza mapato ya ndani kwani kodi zinazotonzwa hivi sasa hazilingani na hali halisi ya kodi za maduka hayo.

Vielvile, Kamati inashauri kodi zitokanazo na Usimamizi wa Mazingira zizingatie athari za Mazingira katika hali ya mabadiliko ya Tabianchi

## HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**:
Kwa kumalizia maoni haya ya Kamati yangu kwa bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, kwa mwaka wa **fedha 2018/2019**, nikushukuru wewe Mheshimiwa Spika bila ya

kumsahau Katibu wa Baraza la Wawakilishi, kwa kuwa nami pamoja na Kamati yangu bege kwa bega, mara zote tunapohitaji ushauri na muongozo wenu, kwa lengo la kuongeza ufanisi katika kazi zetu. Aidha niwashukuru pia watendaji wote wa Afisi ya Baraza, kwa kazi ngumu wanayoifanya kwa kutoa huduma za msingi kwa Waheshimiwa Wajumbe, pamoja na konesha busara na uvumilivu wa hali ya juu kwa lengo la kuhakikisha Baraza linatekeleza kazi zake kwa ufanisi na kwa wakati.

Shukurani zangu za pekee ziwaendelee Wajumbe wa Kamati yangu ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa, kwa kuonesha ushirikiano na uvumilivu, katika kazi zetu za kuisimamia Serikali ndani ya kipindi chote cha mwaka wa fedha **2017/2018**. ni matumaini yangu kuwa, katika kipindi chote hichi, Wajumbe wamejifunza mengi na kutegemea ufanisi zaidi katika mwaka wa fedha unaofuata.

**Mheshimiwa Spika:**

Kwa ruhusa na idhini yako, naomba niwatambue Wajumbe wote wa Kamati hii kwa majina kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1. Mhe. Omar Seif Abeid | Mwenyekiti |
| 2. Mhe. Panya Ali Abdalla | Makamu mwenyekti |
| 3. Mhe. Amina Iddi Mabrouk | Mjumbe |
| 4. Mhe. Ame Haji Ali | Mjumbe |
| 5. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu | Mjumbe |
| 6. Mhe. Mtumwa Suleimn Makame | Mjumbe |
| 7. Mhe. Mussa Ali Mussa | Mjumbe |

Bila kusahu makatibu wetu wawili ambao ni:

| | |
|---|---|
| 1. Ndg. Karima Abdul Wahab | Katibu, na |
| 2. Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu. |

**Mheshimiwa Spika:**

Kwa umakini, uchapa kazi na uzalendo wa Wajumbe wa Kamati hii, Bajeti hii imepitiwa na kuridhiwa, na hatimae kutolewa maoni kwa maeneo ambayo Kamati imekubaliana na Bajeti ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

**Mheshimiwa Spika:**

Baada ya maelezo haya, naunga mkono hoja,
Naomba kuwasilisha,

……………………………

Omar Seif Abeid,
Mwenyekiti,
Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa.
Baraza La Wawakilishi
**Zanzibar.**